JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Boma Road,
S.L.P. 484,
43108SINGIDA,
TANZANIA.

Barua Pepe: rbcsingida@pccb.go.tz.

www.pccb.go.tz

SINGIDA – MEI, 2023

TAKUKURU SINGIDA YAFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 3.5

Ndugu Wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU ni chombo chenye dhamana ya kusimamia Mapambano Dhidi ya Rushwa nchini kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2022. Tunakutana na ninyi waandishi wa habari ili kupitia kwenu, tuuhabarishe umma kuhusu utendaji kazi wetu kama ambavyo imekuwa ikifanyika kila robo ya mwaka. Taarifa inayowasilishwa leo, inahusu utendaji kazi wa ofisi yetu TAKUKURU katika maeneo yote matatu yaani, Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa, Elimu kwa Umma na Uchunguzi kwa kipindi cha **Januari – Machi 2023.**

Ndugu Wanahabari,

Katika eneo la **UZUIAJI RUSHWA** na kwa kuzingatia kwamba miradi ya maendeleo ni mali ya wananchi na Serikali inapeleka fedha nyingi katika eneo hilo, TAKUKURU Mkoa wa Singida imefuatilia utekelezaji wa miradi **Ishirini na nane (28)** yenye thamani ya zaidi shilingi bilioni tatu **(3,507,253,237.63.00)** katika sekta za Elimu na Barabara. Hii inajumuisha miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19 na Serikali Kuu.

Ndugu Wanahabari,

Miradi iliyokaguliwa ilikuwa kama ifuatavyo:-

Miradi ya Elimu iliyokaguliwa ilikuwa saba **(07)** yenye thamani ya shs. 305,906,524.63.

- Miradi ya Barabara iliyokaguliwa ilikuwa mitatu (03) yenye thamani ya shs. 742,786,600.00
- Miradi ya Afya iliyokaguliwa ilikuwa kumi na moja (11) yenye thamani ya shs. 2,036,228,500.00
- Ufuatiliaji wa matumizi ya asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri za Singida, Manyoni, na Ikungi kwa ajili ya makundi maalumu (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu) kiasi cha shs. 422,331,613.00.

Ndugu Wanahabari,

Miradi mitano **(05)** iliyokaguliwa yenye thamani ya **Sh. 1,279,506,500/-** ilikutwa na mapungufu mbalimbalimbali kama ifuatavyo;-

NA	JINA LA MRADI NA THAMANI	YALIYOBAINIKA	HATUA
1	1.Ujenzi Wa Kituo Cha Afya Kisiriri Katika Halmashauri Ya Wilaya ya Iramba. **Shs. 500,000,000/=**	1.Mradi Umechelewa Kukamilika Bila Sababu Zozote za Kitaalamu Kubainishwa. 2.Usimamizi usiokidhi viwango	Wahusika wameshauriwa kuhakikisha mradi unakamilika.
2	Ufuatiliaji wa Asilimia 10 ya vijana,wanawke na walemavu Taarifa ya ufuatiliaji wa matumizi ya asilimia kumi ya mapato ya ndani ya nyaraka kwa ajili ya makundi maalum	-Vikundi kutekeleza miradi kinyume na andiko la maombi. Ucheleweshaji wa nyaraka kwa walengwa. -Ukosefu wa nyaraka katika kikundi husika.	Wahusika walishauriwa kuhakikisha wanafuata sheria kauani na taratibu zilizowekwa.

	(wanawake, vijana na watu wenye ulemavu) katika H/W IKUNGI **-52,000,000/=**	- Vikundi kupewa fedha ndogo tofauti na maombi yao.	
3	Ujenzi Wa Zahanati ya Kijiji Cha Wembere Katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. **-Tshs. 271,000,000/=**	-Mradi Umechelewa Kukamilika Bila Sababu Zozote za Kitaalamu Kubainishwa	Kamati za mradi husika zimeshauriwa kufuata taratibu ili mradi ukamilike kwa wakati.
4	Ujenzi wa Kivuko cha chini cha watembea kwa miguu Kibaoni-MANISPAA ya SINGIDA **Tshs. 388,000,000/=** Mradi unatekelezwa na TANROADS –SINGIDA	-Baadhi ya maeneo yalionekana kuwa na ukamilishaji usiokuwa mzuri.	Wahusika walishauriwa kurekebisha maeneo ambayo yalikuwa hayalidhishi katika umaliziaji wake.
5	3.Ujenzi Wa Zahanati ya Kijiji cha Tutu Katika Halmashauri Ya Wilaya ya Iramba. **-Tshs. 68,506,500/=**	-Mradi haujatekelezwa Kwa Kiwango Kilichotarajiwa na Wananchi Waliochangia Fedha Pamoja na Serikali.	Uchunguzi wa awali umeanzishwa.

Ndugu Wanahabari,

Vilevile, pale ambapo eneo la utendaji au utoaji huduma linaonekana au kulalamikiwa kuwa na viashiria vya Rushwa, TAKUKURU hufanya **uchambuzi wa mfumo** ili kubaini iwapo kuna mianya ya Rushwa na kushauri namna ya kuiziba. Kwa kuzingatia hayo tumefanya **chambuzi tano** za mifumo kama ifuatavyo:-

NA	UCHAMBUZI WA MFUMO	YALIYOBAINIKA	MAKUBALIANO
1	Kubaini mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa michango kutoka kwa wananchi na matumizi yake-H/W MKALAMA	Fedha za michango zinatumika kabla ya kuingizwa kwenye A/C za vijiji -Baadhi ya wananchi hawapewi stakabadhi hasa kama ametoa mchango pungufu -Fedha zinatumika kinyume na madhumuni ya mchango -Wenyeviti wa vitongoji na watendaji wa vijiji wanatumia fedha kwa matumizi binafsi	Fedha ziingizwe kwenye akaunti kabla ya kuanza kutumika. Wananchi wapewe stakabadhi kama taatibu zinavyoelekeza.
2	Chambuzi ya mfumo kubaini mianya ya rushwa katika usimamizi wa fedha za miradi ya maji chini ya kamati za maji za jumuiya za watumia maji. H/W MKALAMA	-Wajumbe wa bodi wanajilipa posho kubwa -Hakuna mwongozo wa viwango vya posho na mishahara -Ukaguzi wa mahesabu haufanyiki	Halmashauri imeahidi kufuatilia suala hili
3	Uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa masoko ya biashara-MANYONI	1. Hakuna sheria ndogo za Halmashauri zinazosimamia uendeshaji wa masoko. 2. Kuna usimamizi hafifu wa soko kupelekea vizimba	Uwishaji wa sheria ndogo ufanyike/sheria ya uendeshaji wa masoko na magulio jandaliwe. Mazingira ya soko yaboreshwe ili kuhamasisha wafanya biashara kufanya biashara zao katika soko

		kuwa wazi, na wafanya biashara wachache kulipa kodi 3. Matumizi hayafuati taratibu, mfano ununuzi wa umeme na malipo ya mhudumu. 4. Baadhi ya mapato hayaingizwi katika mfumo wa mapato, kama mapato yatokanayo na maji na choo. 5. Rejesta ya wafanyabiashara hazihuishwi 6. Kuna malalamiko ya mpango wa uboreshaji wa soko ambapo kila mfanyabiashara atatakiwa kutoa sh 4,000,000/= ili kujengewa kibanda kipya na Halmashauri.	rasmi. Mchakato wa kuwashirikisha wadau (wafanyabiashara waliopo kwenye maeneo yasiyo rasmi), viongozi wa kisiasa, viongozi na watendaji wa serikali uanzishwe ili kupunguza wafanya biashara wanaofanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi na kwenda kwenye maeneo/soko rasmi. Taratibu zifuatwe, wanaostahili kulipa ushuru wa pango wote walipe
4	Uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa vyama vya walimu Manispaa ya SINGIDA	Walimu kukatwa makato ya CWT bila ridhaa yao na bila kujaza fomu TUF 15	Sheria izingatiwe na mwajiri asimkate mwanachama michango kama hakuna uthibitisho wa TUF 15 ambayo inaashiria mwanachama ameridhia makato ya uanachama kwenda chama husika.

		Ukinzani wa maslahi (conflict of interest) mjumbe wa chama kuhusika katika kupitisha notice pale mwanachama anapotaka kujitoa	Utaratibu wa notice kumfikia mwajiri ufuate sheria ili kuondoa mgongano wa maslahi pale ambapo mkuu wa idara anayetakiwa kupitisha notice ni mwanachama na ana nafasi kubwa katika chama kinginge cha walimu.
		Wanachama kuendelea kukatwa kama wanachama wa wa CWT wakati tayari notes ya kujitoa uanachama imewasilishwa ofisi ya mkurugenzi na imekubaliwa kwa kutoa uthibitisho wa barua.	Mwajiri anapopokea barua ya notice ya kusitisha uanachama na kuifanyia kazi anapaswa kusitisha makato ya uanachama mara moja na kuanza kukata makato ya ada ya uwakala kwa mujibu wa sheria.
		Kuwepo kwa mkataba wa uwakala baina ya manispaa ya singida na chama chenye wanachama wengi ambayo haijapitiwa kwa muda mrefu/kuhuishwa	Mkataba upitiwe upya na uendane na maboresho yaliyofanyika katika sheria na kanunni zake pia uhusishe wadau wote wanaohusika na vyama vya walimu vinavyotambulika kisheria ili kuwa na uelewa wa pamoja na kuondoa mgongano na mvutano.
		Mwajiri kukata fedha ya uwakala kwa wanachama na kuwasilisha CWT bila kuwa na akaunti maalumu kwa ajili ya	Chama kinachotakiwa kukata ada ya uwakala kiwe na akaunti tofauti na endapo chama hakina akaunti nyingine kwa ajili ya fedha ya uwakala basi

		fedha ya uwakala.	makato yasitishwe mpaka pale matakwa ya sheria yatakapo tekelezwa
		Watumishi wa serikali kukaimu nafasi ya katibu nafasi ambayo haipo kisheria	i. Viongozi wa vyama vya walimu wakidhi matakwa ya sheria ii. Mwajiri achukue hatua kwa watumishi wanatekeleza majukumu mengine bila kufuata utaratibu wa sheria.

Ndugu Wanahabari,

A. Tumefanya **Warsha nne (4)** kuhusiana na chambuzi za mifumo zilizofanyika kwa kushirikiana na wadau kama ifuatavyo:

a. Kikao cha kujadili mianya ya rushwa iliyobainika katika uchambuzi wa mfumo wa usimamizi wa fedha za miradi ya maji chini ya kamati za maji za jumuiya ya watumia maji.

b. Kikao cha kujadili mapungufu mbalimbali yaliyobainishwa kupitia miradi ya Afya, elimu na Barabara kwa Wilaya ya Singida.

c. Kikao cha kujadili matokeo ya uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa masoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni

d. Kikao cha kujadili kuhusu mapungufu yaliyobainika katika manunuzi ya umma katika miradi ya maendeleo ya halmashauri ya wilaya ya ikungi.

B. Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa maazimio ulifanyika kupitia vikao vifuatavyo ulifanyika:

a. Kikao cha wazazi na kamati ya shule ya msingi bomani halmashauri ya wilaya ya iramba.

b. Vikao vilivyojadili mapungufu mbalimbali yaliyobainishwa kupitia miradi ya Afya, Elimu na Barabara kwa Wilaya ya Singida.

c. Kikao kilichojadili mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa michango kwenye minada.

d. Kikao kilichojadili mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato kwa njia ya POS.

Ndugu Wanahabari,

Programu ya TAKUKURU RAFIKI ni program yenye lengo la kuongeza wigo wa kuwashirikisha wadau kwenye Mapambano dhidi ya rushwa kwa kutumia njia za kuzuia na kupambana na rushwa katika utoaji wa huduma za kijamii na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vikao 10 na wadau vilifanyika katika kata 10 ambapo wadau waliibua kero 140. Ambapo Idadi ya kero zilizotatuliwa ni 41 kamainavyoonekana katika Jedwali:-

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI(TR) KWA KIPINDI CHA FEBRUARI NA MACHI 2023 NGAZI YA MKOA					
NA	**IDADI YA KATA ZILIZOFIKIWA**	**IDADI YA KERO ZILIZOTOLEWA**	**IDADI YA KERO ZILIZOTATULIWA**	**MIFANO YA KERO ZILIZOTATULIWA NA SEKTA YAKE KTK MABANO**	**MAFANIKIO YA TR KATIKA MKOA WAKO**
	10	140	41	-Ubovu wa miundombinu ya Barabara ya karakana –Muhawa. (Kata ya Misuna)	Kero hii imeondoka baada ya kuwasilishwa kwa Meneja wa Wilaya ya Singida na Barabara imechongwa
				Bill za kuwa maji kubwa kuliko matumizi halisi kata ya misuna Singida Manispaa.	Usomaji wa mita sasa unafanyika na wahusika kutumiwa mesaji ya

					kuhakiki usomaji kabla ya ankara kutolewa
				Kero ya uchafu kutokuzolewa kwa wakati katika Dampo la soko la Ikungi	Mkurugenzi wa Ikungi ameishughuli kero hii sasa uchafu unaondolewa kwa wakati.
				Kero ya Boma la zahanati ya vijiji viwili ,lililojengwa kwa nguvu za wananchi wa vijiji vya Zinzigili na Luziluku	Mkurugenzi wa Wilaya ya Iramba amepeleka fedha kiasi cha 50,000,00 kwa ajili ya ukamilishaji boma hilo la zahanati

Ndugu Wanahabari,

Elimu kwa Umma: Elimu kwa umma inafanyika ili kuielimisha jamii kuhusu madhara ya rushwa kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Elimu kwa umma pia inafanyika kwa madhumuni ya kuipa jamii uelewa na hivyo kuihamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa.

TAKUKURU mkoa wa Singida kupitia Dawati la Elimu kwa Umma hutumia mbinu mbalimbali katika kuelimisha kwa kuwashirikisha wanajamii wa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na vijana wa shule za Msingi, Sekondari, Vyuo, Watumishi wa Umma na jamii kwa ujumla.Kazi zilizofanyika ni kama ilivyoainishwa kupitia jedwali hapa chini:

NA	KAZI	UFAFANUZI
1.	Kutembelea na kuziimarisha Klabu za Wapinga Rushwa katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo. Elimu hii ilifanyika kwa kulenga rika la vijana kupitia klabu za wapinga rushwa na kuelimisha wanachama.	Klabu za Wapinga Rushwa zimetembelewa ambapo Jumla ya semina **92** zilitolewa ili kuweka mikakati ya kuziimarisha.
2.	Kushiriki kutoa semina **14** kwenye makundi mbalimbali wakiwemo watumishi wa Umma.	Mafunzo kukuza uelewa juu ya kuzuia vitendo vya rushwa kwa watumishi wa Umma na wananchi kwa ujumla wake.
3.	Mikutano ya hadhara **24** ilifanyika kwa wananchi wa maeneo mbalimbali ndani ya Mkoa wa Singida.	Lengo kuu ni kuwafikia wananchi katika maeneo yao,kuwashirikisha na kusikiliza kero zao pamoja na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwenye maeneo yao.
4.	Kushiriki kwenye vipindi vya redio ambavyo vilirushwa standard redio.	TAKUKURU ilishiriki kutoa vipindi **03** vya redio ambavyo vilihusu wajibu wa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa, makosa ya rushwa na wajibu wa wananchi kulinda rasilimali za nchi
5.	Kushirikiana na wananchi katika kuimarisha ushirikiano wa kutambua kero katika kata	Mikutano **11** ya Program ya TAKUKURU RAFIKI kwenye ngazi ya Mkoa na Wilaya.
6.	Kufanya maonesho 12, TAKUKURU mkoa wa Singida ulifanya maonesho mbali mbali ndani ya Mkoa wa Singida	Pia TAKUKURU ilifanya maonesho hayo **12** kuhusiana kuhamasisha umma katika kuzuia vitendo vya rushwa

Ndugu Wanahabari,

UCHUNGUZI NA MASHTAKA

A. Jumla ya taarifa malalamiko **47** yalipokelewa ambapo taarifa **31** zilihusu vitendo vya rushwa na taarifa **16** hazikuhusu vitendo vya rushwa. Mchanganuo wamalalamiko hayo **47** yaliyopokelewa kisekta ni kama ifuatavyo:

NA	SEKTA	IDADI
1	TAMISEMI	**26**
2	Ardhi	**03**
3	Afya	**01**
4	Mahakama	**02**
5	TARURA	**02**
6	Polisi	**02**
7	Binafsi	**02**
8	Kilimo	**01**
9	Dini	**01**
10	NGO's	**02**
11	Ujenzi	**02**
12	CCM	**02**
13	Bima	**01**
	JUMLA	**47**

B. Malalamiko **31** yaliyohusu rushwa uchunguzi wake unaendelea katika hatua mbalimbali na

C. **Malalamiko 16** ambayo yalibainika hayahusiani na Rushwa walalamikaji walipewa ushauri yanajumuisha sekta zifuatazo.

Na	SEKTA	IDADI
1	TAMISEMI	08
2	Polisi	02
3	Ardhi	03
4	Mahakama	1

5	TARURA	1
6	BINAFSI	1
	JUMLA	**16**

D. TAKWIMU ZA MASHITAKA

NA	**KIPENGELE**	**IDADI**
01	KESI ZILIZOFUNGILIWA	04
02	KESI ZILIZOAMULIWA	01
03	KESI ZILIZOSHINDA	01
04	KESI ZINAZOENDELEA MAHAKAMANI	32
	JUMLA	**38**

Ndugu Wanahabari,

Mkakati wa utendaji kazi TAKUKURU (M) Singida kwa robo ya nne ya mwaka 2022/2023 inayoanzia **Aprili hadi Juni, 2023** ni kufuatilia matumizi ya fedha za Serikali zinazoelekezwa Mkoa wa Singida kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa fedha za Mradi wa **"BOOST"**;Kuzuia rushwa kwenye hutoajiwa huduma, kufanya uchunguzi pale itakapobainika kuwa katika ufuatiliaji huo wa matumizi ya fedha za Serikali zinazoelekezwa Mkoa wa Singida vitendo vya rushwa vimejitokeza; na kuendelea na uelimishaji unaolenga kushirikisha jamii katika uzuiaji wa vitendo vya Rushwa ikiwa ni pamoja na kuendelea kutekeleza Programu ya Takukuru – Rafiki.

WITO:
Ndugu Wanahabari,

TAKUKURU (M) inatoa rai kwa wananchi wote kwa ujumla kujiepusha na vitendo vya Rushwa na kushiriki kikamilifu katika Kuzuia vitendo vya Rushwa vinavyotokea katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma za kijamii na miradi ya maendeleo pia mnatakiwa kutoa taarifa za vitendo vya Rushwa kwa njia mbalimbali ikiwemo:-

i. Kufika Ofisi za **TAKUKURU Singida**(M) na Wilaya Iramba.Ikungi, Mkalama na Manyoni;

ii. Kupiga simu ya bure **113** au kupiga simu kwa Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Singida Namba **0738-150-208**; Mkuu wa Takukuru Mkalama **0738150 212,** Mkuu wa Takukuru Ikungi **0738150 213,** Takukuru Iramba **0738 -150 210** na MkuuTakukuru Manyoni **0738-150 211**

iii. Kutoa ushirikiano kwenye uchunguzi na kushiriki kutoa ushahidi Mahakamani.

Ndugu Wanahabari,

Katika Mkoa wa Singida, kama ilivyo kwa mikoa mingine, kumekuwepo na wimbi la watu wanaojifanya Maafisa wa TAKUKURU na kujipatia fedha kwa kuwahadaa kuwa wanaweza kuwasaidia kupata huduma au nafuu zozote kutoka mamlaka mbalimbali za Serikali.

TAKUKURU (M) Singida inawataadharisha matapeli wote wanaowatapeli au wanaopanga kuwatapeli wananchi kwa kujifanya Maafisa wa TAKUKURU au vyombo vingine vya dola kuacha kwa sababu watakapobainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ikiwemo kuwafikisha Mahakamani.

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU

Imetolewa na:

MKUU WA TAASISI (M)
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA
NA RUSHWA
(TAKUKURU)
MKOA WA SINGIDA

MZALENDO WIDEGE
MKUU WA TAKUKURU (M)SINGIDA
SIMU: 0738150208